



## COUNTY ASSEMBLY OF MOMBASA

### OFFICIAL REPORT

Wednesday, 9<sup>th</sup> May, 2018

The House met at 9:28a.m.

*(Deputy Speaker (Hon. Fadhili Mwalimu) in the Chair)*

### PRAYERS

**Deputy Speaker:** Have your seats, Serjeant ring the quorum bell.

*(Serjeant-At-Arms rung the quorum bell)*

...Hon. Shebe Athuman you are out of order, yeah just don't cross the corridors.

*(Silence)*

...Hon. Ibrahim okay, I thought you are going out. Yes Clerk ascertain if there's quorum?

*(The Clerk confirmed the quorum)*

Okay let's proceed, yes Clerk?

### MOTION

#### ESTABLISHMENT OF A SCHOLARSHIP SCHEME BY THE COUNTY GOVERNMENT

Yes the Chief Whip Hon. Charles Kitula?

**Majority Chief Whip (Hon. Kitula):** Thank you Hon. Speaker. Mr. Speaker I beg to move the Motion on establishment of a scholarship scheme by the County government.

*(Majority Chief Whip (Hon. Kitula) moved the Motion)*

Mr. Speaker Sir AWARE THAT the County government has been providing bursaries to the bright and needy students in the County, aimed at increasing their access to education;

FURTHER AWARE that various institutions and well wishers have also been providing scholarships to the needy students who have performed exemplary in the County;

CONCERNED that despite the disbursement of the bursaries from the County government and the scholarships from the companies, a number of deserving students especially from public primary schools have been left out due to a myriad of reasons for instance, the rigorous cut – off mark of 350 needed for one to gain scholarship for high school admission;

I therefore urge this Assembly to RESOLVE:

1. That the County government set up a scholarship scheme for the needy and bright students from the County especially from public primary schools, who are joining high school with a pass mark of 300.

2. That the County government partner with companies from within and outside the County that do not offer scholarship programmes in the County so that County government can accommodate the anticipated large number of needy students.

Mr. Speaker may I ask Hon. Nyiro to second my Motion.

**Hon. Nyiro:** I second Mr. Speaker.

*(Question proposed)*

**Deputy Speaker:** I now propose a question that the Motion on Establishment of Scholarship scheme by the County government be discussed in this Honorable House.

*(Question proposed and agreed to)*

Yes Hon. Kitula?

**Majority Chief Whip** (Hon. Kitula): Ahsante sana Mheshimiwa Spika na vile vile ningependa kuwashukuru Waheshimiwa wenzangu kuweza kujadili hoja hii yetu ya leo. Mheshimiwa Spika ni dhahiri shahiri ya kwamba hivi sasa watoto wanaopata ufadhili kutoka katika Kampuni za kuweza kuwekeza fedha, kama vile Cooperative, Equity na vile vile KCB wanaweza kuchukua wanafunzi walioweza kupitisha alama ya zaidi ya 350.

Lakini kusema kweli Wabunge wenzangu na vile vile Mheshimiwa Spika kuna wanafunzi ambao wanasoma katika shule za serikali ambao wameweza kupata alama ya 300, hao huwa wanapata kero, hawajui wataelekea wapi?

*(Power Interruption)*

*(Silence)*

**Deputy Speaker:** Yes proceed.

**Majority Chief Whip** (Hon. Kitula): Ahsante Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Spika wanafunzi hawa ambao waliweza kupata alama ya 300 huwa hawajui wataweza kupata msaada kwa nani, maana kama unavyofahamu sisi ni viongozi tulioweza kuchaguliwa na katika hali ya kuweza kupata basari huwa haiangalii umepata alama ngapi bora tu uwe na ushirikiano na yule Mbunge maana sisi Serikali ya Kaunti ni watu tu wa kuweza kuwakilisha majina yenu katika ofisi zile za CDF na kuwakilisha majina katika ofisi za Kaunti na kuweza kutoa tu namba ya account lakini hatuangukii yule mwanafunzi ameweza kupata alama ngapi?

Mheshimiwa Spika lakini sisi kama Wabunge leo hii tukiweza kujadiliana na kuweza kuwawekea mpangilio watoto hao ambao watakosa kupata alama ya 300 itakuwa rahisi kama sisi Wabunge kuweza kuhakikisha kwamba endapo kama unawakilisha eneo lako, kuna wanafunzi ambao wamepata alama ya zaidi ya 300 ni kuchukua majina yake na kuweza kupeleka katika serikali ya Kaunti na kuweza kuhakikisha kwamba amepata *scholarship* kuanzia kidato cha kwanza hadi kidato cha nne na hapo haitakuwa mwisho. Kwa sababu lazima tuangalie hawa wanafunzi ambao tumeweza kuwapatia *scholarship* wanaendelea vipi; pia vile vile serikali ya Kaunti iweze kuhakikisha wanapata elimu bora ya chuo kikuu.

Kwa hivyo Wabunge wenzangu ningependa sana kuweza kutilia mkazo maana sisi kama bajeti yetu ya basari imeweza kuzingatia sana pesa chache zaidi Mheshimiwa Spika lakini sisi tunawafadhili na makampuni mengi yako tayari kuweza kusaidia wanafunzi wetu lakini tu bora tuweze kuwafuata na kuongea nao na kuweza kuwapatia idadi kamili hasa wanafunzi hawa ambao twaweza kuwapatia motisha kwamba endapo utapata alama 300 basi atakuwa anapata uhakika wa kuweza kusomeshwa kuanzia kidato cha kwanza hadi kidato cha nne.

Kwa hivyo nalihimiza Bunge hili hasa Waheshimiwa wenzangu tuweze kuanzisha rasmi mpango huu hapa katika serikali yetu ya Kaunti na kuweza kuwapatia motisha wanafunzi wetu kwamba endapo mwanafunzi yeyote ataweza kupata alama 300 ataweza kusimamiwa na serikali ya Kaunti kuanzia kidato cha kwanza hadi kidato cha nne na vile vile kuweza kuzingatia elimu yake ya chuo kikuu na vile vile pia sisi kama Wabunge tutapatiwa majukumu ya kuweza kuwaleta wanafunzi hao katika idara husika. Ahsante sana.

**Deputy Speaker:** Yes Hon. Ibrahim?

**Hon. Omondi:** Thank you very much Mr. Speaker Sir and I would like also to add my voice to this very important Motion. Mr. Speaker we all know that most of us here in this House are here because of our educational background and it is very important to acknowledge that education is very important as far as our country is concerned especially our County is concerned.

Mr. Speaker Sir you know that Mombasa County; almost half of Mombasa County learners, most of them are not able to get quality education due to some of the reasons, this is one of the main reasons why you will find that in Mombasa County the illiteracy rate is very high, lack of funds which can actually make these students advance to the next stages and therefore I just want to congratulate the Hon. Members Hon. Charles Kitula who thought wise to come up with this Motion at this particular time and am a victim of this. I remember very well when I started my education my parents passed through a very difficult time to ensure that I have attained the best education as I can and therefore I could be the last person to oppose this particular Motion.

Another reason that I want to support this particular Motion being the Chairman of Education I have had very many delegations into my office and most of them are attributed towards this particular kitty, that is the bursary particularly for the pupils who do well in primary schools but they are not able to continue with their education due to lack of funds and therefore I just want to support it but again it is very important for the Members in this particular House and stakeholders involved in this that as much as we are supporting this Motion it is also very important that this one should meet the threshold. We do not want a situation that we pass this particular Motion and after passing the bursaries are availed but again the cartels surrounding this kitty make this particular thing dysfunctional at the end of it all.

Mr. Speaker Sir am saying this because at this particular time we have faced a very difficult moment especially the MCAs on the ground on the issue of bursary, even as we are speaking we do not have bursary on the ground.

And that is why I want to say that we support the Motion, it is very important that the enforcement is urgently done and should be moving very fast to ensure that this particular kitty is availed at the right time when we most or urgently need it, it must be available. Thank you very much Mr. Speaker Sir I stand firm and I support this Motion. Thank you.

(Applause)

**Deputy Speaker:** Yes Hon. Faith?

**Hon. (Ms.) Boniface:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika ningependa sana kuunga mkono Mswada huu ambao umeletwa siku ya leo lakini kuna mambo muhimu ambayo yafaa tuzingatie kama jukumu la Kaunti lenyewe limetushinda mambo ya ECDs na Polytechnics ukiangalia kila mtu yualia. Mheshimiwa Spika kulingana na *survey* ambao umefanywa na Uwezo Kenya waliweza kudhihirisha ya kwamba watoto wa darasa la nane wanashindwa kusoma kazi ya darasa la pili na watoto wa darasa la tatu wanashindwa kusoma vitu vya darasa la pili na hiyo ni kumaanisha msingi wa mtoto haukuwa sawa. Kwa hivyo tungezingatia kwanza msingi wa mtoto uwe sawa ndio tuzingatie mambo ya *scholarship* Mheshimiwa Spika siku hii ya leo watoto wameenda shuleni Mombasa Kaunti hatujatoa basari hii *scholarship* itatoka wapi kama basari zenyewe za pesa chache hatuwezi zipata?

Mheshimiwa Spika sioni haja ya kuendelea kupanua wanaume matumbo, watu wengine wakiumia kama kweli utapita huu Mswada japokuwa hili Bunge huwa naona twapitisha Mswada hauendi mahali japokuwa itapita ni kuwe na misingi kabambe ambayo itahakikisha zile pesa zimefikia wenye wanapaswa. Ahsante sana Mheshimiwa Spika.

(Applause)

**Deputy Speaker:** Yes Hon. Mwamwiri?

**Hon. Athman Mwamiri:** Ahsante Mheshimiwa Spika nasimama kwa nia ya kuunga mkono hoja ya ndugu yangu Mheshimiwa Kitula. Mheshimiwa Spika asilimia kubwa ya wakaazi wa Mombasa ni walala hoi na ina walazimu watoto wao kusoma katika shule zetu za umma hivyo basi changamoto wanazopitia katika shule za umma haziwezeshi kupata alama za juu kulinganisha na sehemu za taifa hili ama baadhi ya chuo ama shule katika maeneo yetu ya Mombasa mfano shule za ubinafsi watoto wanaosoma pale ni watoto walala hoi mandhari yako sahihi mazingira yanaruhusu na karibu kila kitabu na maktaba iko pale kuwawezesha kuzingatia na kufikia alama zinazostahiki lakini tukitembelea mashule yetu sisi kama viongozi ni masikitiko watoto wetu zile shule wanasomea mazingira yale hayaruhusu abadan kwa mtoto kupata hata alama 300. Kwa hiyo kwa kiwango cha 300 pia hatutakuwa na idadi kubwa vile kwa sababu wengi na tukiangalia alama ya mkato ya shule zetu ni alama 217 hadi 250 kwa hio ni watoto watatu hadi sita kwa kila shule wenye wana uwezo wa kufikisha alama ya 300. Hivyo basi kuweka kiwango cha 350 ni kuwahujumu watoto wa maskini wa Kaunti ya Mombasa na kupeana nafasi kwa watoto wa walala hoi kwa shule za kibinafsi kupata nafasi ile na *scholarship* zile kuweza kuwasomesha hali ya kuwa wazazi wao wanao uwezo.

Kwa hivyo basi ni jukumu letu kama Kaunti kwanza tuweke mfuko huu wa *scholarships* mbali na basari kwa sababu basari zinatoka kimsimu na zinasaidia padogo ikizingatia shule zetu za upili zilivyo juu na ni jukumu letu kama Kaunti ya Mombasa tupitishie na tutenge kiwango cha fedha kitakacho wawezesha watoto wa kimaskini wenye jitihada na juhudi kufikisha alama 300 kuweza kupata *scholarship* zitakazo wawezesha kukimu mahitaji yao chuo kuanzia kidato cha kwanza hadi kidato cha nne na ikilazimu kujiunga na vyuo vya upili kadhalika ili tujihesabie kuwa Kaunti ya Mombasa tuko na idadi kadha za ma Engineer ambao ni vijana vyetu, tuko na madaktari wa ngapi.

Kama Kaunti tumewafadhili na kuwawezesha kusoma ndipo tunapojenga hospitali tunajua madaktari wapo wa kuwapeleka lakini unakuta hospitali zetu zinakosa wahudumu kwa sababu hatujawezesha ama wekeza katika suala zima la elimu. Kwa hivyo naunga mkono suala hili tupunguze kiwango cha alama kutoka 350 hadi 300 isiwe tu suala la basari bali tuweke mfumo wa *scholarship* kusaidia wazazi wetu wa kimaskini na mikakati kabambe iwekwe hizi basari zenye zimekuwa zikiwekwa je masikitiko unakuta Wodi moja inapata basari 100 zengine hazijulikani zimeishia wapi? Kwengine 200 hazina mfumo mahsusi ambazo zinawezesha kufuatilia na kujua waliofaidika ni kina nani.

Mheshimiwa Spika fomu zinakuja na *Ward Administrator* anapeana na kamati yake ya maendeleo Mheshimiwa ukipata bahati utapewa fomu 20 ama uambiwe ulete watu na ukifika fomu ni 15 zinazogawanywa. Kwa hivyo mbali na kutengwa na kima hiki kadhalika kuwe na mikakati kabambe yatakayoonyesha usawa na kufaidisha wale wanaostahiki. Ahsante Mheshimiwa Spika.

(Applause)

**Deputy Speaker:** Yes Hon. Ali Shariff?

**Hon. Ali Shariff:** Ahsante Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hoja ilioletwa na Mheshimiwa mwenzangu Kiranja wa Bunge Charles Juma Kitula. Mheshimiwa Spika mimi kama Naibu wa Kamati ya Elimu nimeamka kuunga mkono Hoja hii kwa sababu sisi Kamati ya Elimu tunaletewa hoja nyingi kama hizi hususan mambo ya basari na mambo ya udhamini wa wanafunzi. Mheshimiwa Spika hali ya uchumi iko chini, wazazi ni masikini, kwa hivyo naomba Kaunti ichukue jukumu la kusomesha wanafunzi wa shule ya upili...

(Applause)

...Mheshimiwa Spika naona ulipouliza nani anapinga Hoja hii sikuona mtu aliopinga kila mtu alisema *Ayes*, kwa hivyo sioni haja ya kuendelea mvua yaendelea tupe nafasi twende mashinani tukasaidie watu huko. Ahsante sana.

(Applause)

**Deputy Speaker:** So you are proposing an adjournment Motion? Yes Hon. Feddis?

**Hon. (Ms.) Mbura:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi hii, pia mimi naunga mkono Hoja hii ilioletwa mbele yetu na ningeomba pia wenzangu tuweze kuiunga mkono, kwa sababu kusema kweli watoto masikini ni wengi na wengi wamevunjika mioyo kwa sababu wanajua wanasoma ikifika mwisho wa kusoma hawaendi mahali popote lakini Kaunti itakapochukua hili jukumu kwamba laweza toa udhamini wa masomo kuanzia shule ya upili mpaka kwenye vyuo vikuu mpaka vyuoni nafikiri wale watoto watatoa ile ari ya kwamba mimi nikisoma siendi mahali popote.

Kwa hivyo mimi naunga mkono asilimia 99 nimeacha tu moja na saa hii Mheshimiwa Spika kuna vijana wengi sana waliomaliza kidato cha nne wako na B, wako na C+, wako na A lakini kusema kweli hawajaenda mahali popote ambapo udhamini huu ukitoka basi hakika hatutaacha vijana katika vizazi vinavyokuja kuranda randa kama saa hii. Hivyo basi mimi naunga mkono na jambo hili tunapolipitisha basi hata sisi Wajumbe hapa tuhusishwe kwa sababu sisi ndio tunajua kule mashinani ni familia gani iko chini, ni familia gani ni masikini? Lakini kama watatumia wale *Ward Administrators* na kutuacha sisi basi hili jambo kusema kweli halitaenda mahali popote ama watakao faidika ni wale ambao wana uwezo.

Kwa hivyo naunga mkono na mikakati pia iwekwe sisi MCA tuhusishwe. Ahsante sana Mheshimiwa Spika.

(Applause)

**Deputy Speaker:** Yes Hon. Nyiro?

**Hon. Nyiro:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika nitakuwa mtovu wa nidhamu sana kama mwalimu kama jambo hili nitasita kukutilia pondo na kwa sababu hiyo kwanza nataka nitoe kongole kwa Mheshimiwa Kitula ambaye amefikiria zaidi ya umri wake na niseme kwamba Jumba hili kama nilivyosema jana ni kwamba majukumu yake yote ni matukufu kwa sababu Wang'eng'e walisema, "*Service to humanity is service to God*", ukipewa jukumu la kuhudumia mwanadamu umepewa jukumu la kumuhudumia Mungu. Kwa hiyo ukienda Nairobi ukisema kuwa watoka Mombasa hawatarajii kwamba uwe na tajriba yoyote ya kujua mambo ya kusoma na nafikiri kwa sababu tuko na serikali sasa huku Mombasa ni vizuri tuone kwamba hali hii tutaigeuza vipi? Kwa sababu sisi twajulikana ni Waswahili tu wa *ndoo* na mambo ya kimsingi ya elimu hatuwezi kuyazingatia.

Mambo haya tunayoyafanya hapa si mwanzo kwa sababu wakati mwengine ukitaka kufanya kitu hebu angalia mwenzako na mimi nina uzoefu sana kwenda Kaunti ya Kwale; Mheshimiwa Spika kama sijakosea Kwale Kaunti wamepiga hatua zaidi sisi twaanza na watoto wa shule za msingi kuwapeleka sekondari wao wamechukua *professionals* sasa hivi tunavyoongea wako na vijana wao kadhaa wengine wako India, wengine wako Ujerumani wanasomea udaktari na lengo lao kuu ni kwamba Kwale wawe na *professionals* ambao wamewajenga wenyewe ili wakiwaambia kuwa watafanya kazi Kwale pekee yake iwe ni sheria ambayo itakuwa inabana vizuri. Kwa sababu kama Kaunti imekusomesha utakuwa huna budi ila kufanyia kazi Kaunti na baada ya miaka ijayo utashangaa kwamba watu wanatoka Mombasa wakienda kufanyiwa upasuaji wa ubongo, wa moyo Kwale Kaunti kwa sababu ya nini wameangalia mbele wanataka kutengeneza *professionals* wawe na madaktari na wahandisi ambao wamewajenga wenyewe.

Kwa hivyo jambo hili tunajua kwamba majukumu ya shule hususan ya msingi na upili ni majukumu ya serikali kuu lakini wale wananchi ambao wanasababisha kuwe na serikali hapa Mombasa ni wananchi wa Mombasa Kaunti na Mheshimiwa Kitula ametoa hoja ya kwamba serikali ya Kaunti inaweza kuungana na *private companies* ama watu binafsi ambao wanaweza kuchangia katika hundi hili ili iwe kwamba, maanake kuna *well-wishers* wengi ambao wanasaidia vijana na sasa kama serikali ya Kaunti itakuwa imekuja na mfumo mahususi basi kila mwenye kutaka kusaidia atakuwa anaelekezwa kwenye akaunti ile ili waweze kueleza pesa zao ili zisaidie wanafunzi na mbali na hiyo pia tuko na pesa za basari zile zile basari ambazo tunazipeana tunaweza tukapata fungu pale tuziekeze katika ile hazina ya *scholarships*.

Nikikupa mfano Mheshimiwa Spika kwamba kwangu kuna kijana ambaye alipata alama 378 na akaitwa Kenyatta, Kenyatta ni shule ya kitaifa na ninavyoongea hivi sasa yuko nyumbani kwa sababu alishindwa kwenda Kenyatta na akashindwa kuingia hata zile shule ambazo ziko mitaani kwa sababu hana baba wala mama anayemuangalia ni Mheshimiwa Nyiro amlipie karo. Ni masikitiko kwa sababu katika ile shule ya Kashani yeye ndie alikuwa mwanafunzi wa kwanza na mpaka sasa yuko nyumbani na alimaliza kusoma mwaka jana.

Lengine Mheshimiwa Spika ni kwamba katika hali hii ya kutafuta hii fedha tunajua kwamba Kaunti ya Mombasa ukitaja fedha basi ni kama umegusa jicho la mtu, kwa sababu utaelezwa kanuni nyingi na sheria nyingi lakini tunalosema kama Bunge tunahitaji kusaidia wanafunzi wanaofanya vyema na wanabaki manyumbani hili ndilo tunalosema.

Sasa ikiwa sheria hairuhusu tunasema papatikane pesa wanafunzi wanaofanya vyema waende wakasome kwa sababu zile sheria nyingi tukizifuatilia zitatushinda hata kunywa maji. Mheshimiwa Spika kuongezea na hilo alama ambayo Mheshimiwa Kitula ameiweka ya 300 ni alama nzuri kwa sababu unaweza kushangaa katika *Sub-County* nzima mwanafunzi wa kwanza ana alama ambazo hazifiki hata 300, 290, 280, 301 sasa...

*(Power interruption)*  
*(Silence)*

...sasa tukizingatia kwamba shule kama vile Mheshimiwa Mwamwiri alivyosema kwamba ni shule zetu za umma hali ya masomo yako chini sana.

*(Interruption)*

**Deputy Speaker:** Mr. Nyiro just waits for some few minutes, because it is being recorded.

**Hon. Nyiro:** I thought it is recorded.

**Deputy Speaker:** You can but it is not clear, we need it all recordings to be recorded for our benefit and the benefit of the County and due to power failure we shall adjourn until today afternoon and we will proceed from where we are in the afternoon. So the Assembly stands adjourned until today 2:30p.m.

The House rose at 10:04a.m.